Ayalandi


An Roinn Dlí agus Cirt,
Gnóthaí Baile agus Imirce
Department of Justice,
Home Affairs and Migration

euaa
EUROPEAN UNION
AGENCY FOR ASYLUM

# UNACHOHITAJI KUJUA KUHUSU KANUNI ZA USIMAMIZI WA HIFADHI NA UHAMIAJI

Aina ya A

**WAOMBAJI WA ULINZI WA KIMATAIFA**




SWAHILI

# YALIOMO


kwa nini unapokea kitabu hiki cha maelezo? 3

Ulinzi wa kimataifa ni nini na nani anaweza kuupokea? 3

Kanuni za Usimamizi wa Hifadhi na Uhamiaji ni nini? 4

Uhamishaji ni nini? 5

Haki zako unapongojea uamuzi kuhusu ni nchi gani ya EU+ itakayochunguza ombi lako 6

Unapaswa kukaa wapi unapongojea uamuzi kuhusu ni nchi gani ya EU+ itakayochunguza ombi lako? 8

Unatarajiwa kufanya nini katika mchakato huu? 8

Ni nyaraka zipi unazopaswa kuonyesha? 9

Kwa nini unalazimika kutoa alama zako za vidole na picha? 10

Madhara yake ni yapi ikiwa hutatimiza wajibu wako? 11

Kuzuiliwa ni nini? 12

Mamlaka huamuaje, nchi ya EU+ itakayochunguza ombi lako? 13

Unaweza kufanyiwa usaili ili kusaidia kuelewa ni nchi gani ya EU+ itakayochunguza ombi lako 16

Je, usaili hufanyika kila mara? 18

Ni ushahidi gani unaweza kutoa ili kuthibitisha kuwa una familia katika nchi nyingine ya EU+? 19

Mchakato utachukua muda gani? 20

Vitakuwaje ikiwa tayari umeomba ulinzi wa kimataifa katika nchi nyingine ya EU+? 21

Nini hutokea baada ya uamuzi kufanywa? 22

Unachohitaji kujua kuhusu utaratibu wa rufaa (wakati athari ya kusitisha utekelezaji na rufaa ya msingi zimetenganishwa 24

Ni data gani binafsi zitakazokusanywa? 25

Una haki gani kuhusiana na data zako za kibinafsi? 25

## KWA NINI UNAPOKEA KITABU HIKI CHA MAELEZO?

Umeomba ulinzi wa kimataifa (pia unaojulikana kama hifadhi) katika mojawapo ya nchi 31 za EU+. Hii inamaanisha kuwa sasa wewe ni mwombaji wa ulinzi wa kimataifa. Inawezekana kuwa nchi nyingine ya EU+ ndiyo yenye jukumu la kuchunguza ombi lako. Sasa unasubiri uamuzi huo.

Ni muhimu kuelewa jinsi nchi za EU+ zinavyoshirikiana kwani hii inaweza kuathiri ni nchi gani itakayochunguza ombi lako.Utapata taarifa zote muhimu katika brosha hii.

## ULINZI WA KIMATAIFA NI NINI NA NANI ANAWEZA KUUPOKEA?



Unaweza kuhitaji ulinzi wa kimataifa ikiwa huwezi kurudi nchini kwako kwa sababu unaogopa mateso au unakabiliwa na hatari halisi ya madhara makubwa. Hii inamaanisha, kwa mfano, kwamba maisha yako au uhuru wako yangehatarishwa na mamlaka za nchi yako hazitakulinda dhidi ya hatari unayokabiliwa nayo.

Utapokea maelezo zaidi kuhusu ulinzi wa kimataifa katika brosha tofauti.

**Sasa uko nchini  Ayalandi ambayo ni mwanachama wa Umoja wa Ulaya [EU+].**
**Nchi wanachama wa EU+ ni:**

Nchi 27 wanachama wa Umoja wa Ulaya (EU): Austria, Ubelgiji, Bulgaria, Kroatia, Saiprasi Jamhuri ya Czech, Denmark, Estonia, Ufini, Ufaransa, Ujerumani, Ugiriki, Hungaria, Italia, Latvia, Lithuania, Luksemburgu, Malta, Uholanzi, Poland, Ureno, Jamhuri ya Ireland, Romania, Slovakia, Slovenia, Uhispania, Uswidi na

Nchi nyingine 4: Iceland, Liechtenstein, Norway na Uswisi.

# KANUNI ZA USIMAMIZI WA HIFADHI NA UHAMIAJI NI NINI?




Nchi za EU+ zimekubaliana juu ya sheria ya kawaida inayoitwa Kanuni ya Usimamizi wa Hifadhi na Uhamiaji (AMMR). Sheria hii husaidia kuamua ni nchi gani inawajibika kuchunguza maombi ya ulinzi wa kimataifa. Sheria hii pia inaruhusu nchi za EU+ kusaidiana ikiwa nchi moja itapokea maombi mengi sana kwa wakati mmoja.

Unahakikishiwa kwamba moja ya nchi za EU+ itachunguza ombi lako, lakini huwezi kuchagua ni nchi gani ya EU+ itakayohusika. Nchi itakayochunguza ombi lako itaamuliwa kulingana na sheria za AMMR.

Ikiwa kuna chochote katika brosha hii ambacho huelewi, unaweza kuuliza afisa wa uhamiaji.



Kwa sasa, nchi za EU+ zinaamua tu ni ipi kati yao ndiyo yenye jukumu la kuchunguza ombi lako.

Ikiwa itaamuliwa kuwa nchi nyingine ya EU+ ndiyo yenye jukumu la kuchunguza ombi lako, utahamishwa kwenda nchi hiyo.

# UHAMISHAJI NI NINI?



Moja ya njia ambazo nchi za Ulaya zinaweza kusaidiana ni kwa kuchukua jukumu la:

- waombaji wahifadhi wanaoishi kwa sasa katika nchi nyingine ya Ulaya
- watu ambao hivi karibuni wamepewa ulinzi wa kimataifa katika nchi nyingine ya Ulaya.

Hii inajulikana kama uhamishaji.

Ikiwa unafikiriwa kwa ajili ya uhamishaji, utapokea brosha yenye maelezo zaidi kuhusu mchakato huu, ikiwemo ni nchi zipi za Ulaya zinazoshiriki katika uhamishaji, yenye kichwa cha **'Unachohitaji kujua kuhusu uhamishaji'.**

**MAMBO YA KUZINGATIA!** Ikiwa utachaguliwa kuhamishwa, huwezi kujichaguria nchi unayohamishiwa

## HAKI ZAKO UNAPONGOJEA UAMUZI KUHUSU NI NCHI GANI YA EU+ ITAKAYOCHUNGUZA OMBI LAKO



Ikiwa unaomba ulinzi wa kimataifa kwa mara ya kwanza, una haki ya kupata **ushauri wa kisheria** bila malipo. Unaweza kuomba hili wakati wowote kutoka kwa mamlaka.

Mshauri wa kisheria atakujulisha kuhusu haki zako na atakusaidia katika mchakato. Ikiwa tayari umelipa kuajiri mshauri wa kisheria, mamlaka hawawezi kukupatia ushauri wa kisheria bila malipo. Ushauri wa kisheria unaweza kutolewa katika mazingira ya kikundi, lakini mshauri hatashiriki taarifa zako za faragha na watu wengine.

Unaweza kuomba taarifa na ushauri wa kisheria katika Kituo cha Mapokezi cha Citywest katika Huduma ya Ushauri nasaha ya Bodi ya Msaada wa Kisheria ya Citywest.



Unaweza kuomba mkalimani wa kiume au wa kike na afisa wa kesi ikiwa hilo litaifanya iwe rahisi kwako kuzungumzia hali yako. Mamlaka zitaheshimu ombi lako pale inapowezekana.

9



Una pia haki ya kuomba taarifa mpya kuhusu utaratibu wa kuamua ni nchi gani ya EU+ itakayochunguza ombi lako. Ikiwa ungependa kuomba taarifa mpya, unaweza kuwasiliana na mamlaka kupitia kwa kutuma barua pepe kwa contact@ipo.gov.ie.




Una haki ya kuwasiliana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) katika hatua yoyote ya mchakato wa kuomba hifadhi.

UNHCR hulinda maslahi na haki za wanaotafuta hifadhi na wakimbizi.

Maelezo ya mawasiliano ya UNHCR na taarifa kuhusu mchakato wa kuomba hifadhi yanaweza kupatikana kwenye tovuti ya UNHCR: https://help.unhcr.org/.

**Unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu msaada na huduma utakazopokea katika brosha tofauti.**

## Unapaswa kukaa wapi unapongojea uamuzi kuhusu ni nchi gani ya EU+ itakayochunguza ombi lako?



- Una wajibu wa kukaa katika nchi hii wakati uchunguzi unafanyika.
- Unaruhusiwa kusafiri kwenda nchi nyingine ya EU+ tu ikiwa utapewa ruhusa ya kufanya hivyo na mamlaka.
- Ikiwa mamlaka yataamua kwamba nchi nyingine ya EU+ itachunguza ombi lako, mamlaka yatapanga safari yako kwenda nchi hiyo.

## UNATARAJIWA KUFANYA NINI KATIKA MCHAKATO HUU

unapaswa:

- ✓ kubaki katika nchi hii wakati ombi lako linasajiliwa.
- ✓ Ikiwa umetolewa visa au kibali cha makazi hapo awali, omba hifadhi katika nchi iliyokupa viza hiyo mara tu utakapowasili huko.
- ✓ Wasilisha nyaraka zote za kitambulisho ulizonazo ili kuthibitisha utambulisho wako.
  Ikiwa ulikuwa na hati ya kitambulisho lakini hauna tena, bado unapaswa kuwajulisha mamlaka kwamba ulipewa moja hapo awali na serikali ya nchi yako.
- ✓ Waambie mamlaka kila wakati uliposafiri kwenda nchi nyingine ya EU+
- ✓ Waambie mamlaka ikiwa umekaa katika nchi ya EU+ bila ruhusa.
- ✓ Wajulishe mamlaka kuhusu familia yoyote ya karibu uliyo nayo katika nchi nyingine ya EU+.

**MAMBO YA KUZINGATIA!** Kwa mujibu wa sheria, unalazimika kutoa alama zako za vidole na kupigwa picha.

## NI NYARAKA ZIPI UNAZOPASWA KUONYESHA?

Wasiliana na mamlaka nyaraka zote ulizonazo kuhusu:




- utambulisho wako (cheti cha kuzaliwa, pasipoti, kadi ya utambulisho).



- Wanafamilia wa karibu katika nchi za EU+ (nyaraka rasmi, uthibitisho kuwa mnawasiliana).




- makazi ya awali katika nchi za EU+ (kwa msingi wa kibali cha makazi, viza au kupata diploma ya shule au chuo kikuu).

Tolea taarifa hii haraka iwezekanavyo. Kwa njia hii, nchi ya EU+ inayohusika na ombi lako inaweza kutambuliwa haraka zaidi.

## KWA NINI UNALAZIMIKA KUTOA ALAMA ZAKO ZA VIDOLE NA PICHA?



Mamlaka katika nchi hii zitachukua alama zako za vidole na kupiga picha yako. Data hii, pamoja na taarifa kuhusu utambulisho wako na taarifa nyingine muhimu, itatumwa kwenye hifadhidata ya Ulaya inayoitwa Eurodac.

Hifadhidata hii inatumiwa na nchi zote 31 za EU+ ambazo zinaweza kuchakata data zako ili kupata taarifa zako. Ikiwa utahamia nchi nyingine ya EU+ bila ruhusa na vidole vyako vitafanyiwa uchukuaji tena, data zako zote zilizohifadhiwa katika Eurodac zitaonekana na mamlaka ya nchi hiyo.

Maelezo zaidi kuhusu hifadhidata ya Eurodac yanapatikana katika brosha tofauti.




## MADHARA YAKE NI YAPI IKIWA HUTATIMIZA WAJIBU WAKO?



Usiposhirikiana na mamlaka, hii itakuwa na madhara kwa ombi lako.

Usipotoa alama zako za vidole, mamlaka wanaweza kuhitimisha kuwa huna tena nia ya hifadhi barani Ulaya. Watakoma kuchunguza ombi lako, jambo ambalo litamaanisha kuwa hutakuwa tena na haki ya kubaki katika nchi hiyo.

ikiwa utasafiri kwenda nchi nyingine ya EU+ bila ruhusa au ukiomba ulinzi wa kimataifa katika nchi tofauti ya EU+, kuna uwezekano utarudishwa kwenye nchi ya EU+ inayohusika na kuchunguza ombi lako.




Ukiwa katika nchi ya EU+ isiyo ile unayotakiwa kuwa, uhuru wako unaweza kupunguzwa na unaweza kupokea msaada mdogo.

## KUZUILIWA NI NINI?

Kuwekwa kizuizini kunamaanisha kwamba umewekwa katika kituo maalum ambacho huwezi kuondoka kwa uhuru. Mamlaka lazima iwe na sababu halali ya kukuzuia. Lazima wawe na uhakika kwamba hakuna chaguo jingine linalowezekana katika kesi yako. Mamlaka yatatathmini hali yako binafsi kabla ya kufanya uamuzi.  Sababu za kuwekwa kizuizini zinaweza kuwa, kwa mfano:



- nyanja muhimu za ombi lako la hifadhi (kwa mfano utambulisho wako) haziwezi kuthibitishwa bila kukuweka kizuizini
- hujaheshimu wajibu wa kukaa mahali maalum, au kuna hatari utatoroka tena na mamlaka haitaweza kukufikia
- umepokea uamuzi wa kuhamishiwa kwa nchi ya EU + inayohusika na kuchunguza ombi lako la hifadhi na kuna hatari utatoroka kabla ya kuhamishwa.
- una sababisa maswala ya usalama.

.

Ikiwa utazuiliwa, unaweza kupinga uamuzi huo na kuomba msaada wa kisheria na uwakilishi bila malipo.

.

**MAMBO YA KUZINGATIA!** Ikiwa utazuiliwa, unaweza kupinga uamuzi huo na kuomba msaada wa kisheria na uwakilishi bila malipo..

## MAMLAKA HUAMUAJE, NCHI YA EU+ ITAKAYOCHUNGUZA OMBI LAKO?

Ikiwa hii ni ombi lako la kwanza la ulinzi wa kimataifa katika nchi ya EU+, kuna sababu kadhaa kwa nini nchi fulani ya EU+ inaweza kuwa na jukumu la kuchunguza ombi lako.

### 1) Uhusiano wa kifamilia



Sababu ya kwanza na muhimu zaidi ni kwamba mwanafamilia wa karibu tayari amepewa ulinzi wa kimataifa au kwa sasa analituma ombi la ulinzi wa kimataifa katika nchi nyingine ya EU+, na unapaswa kuungana nao tena kabla ya ombi lako la ulinzi wa kimataifa kuchunguzwa.

Wanafamilia wa karibu wanachukuliwa kuwa ni:

- mume wako au mke wako
- mpenzi wako asiyeolewa/kufunga ndoa ambaye mna uhusiano imara
- mtoto wako (chini ya umri wa miaka 18 na asiyeolewa/kufunga ndoa).

**MAMBO YA KUZINGATIA!** Unapaswa kuweza kuthibitisha haraka iwezekanavyo kwamba ulikuwa na uhusiano na mtu huyo kabla ya kuingia katika eneo la nchi za EU+. Kipindi hiki kinaweza kujumuisha safari kutoka nchi yako.

Ikiwa una mwanafamilia anayeishi katika nchi nyingine ya EU+, njia bora ya kutoa taarifa ni kwa kujaza fomu inayoitwa **'kiolezo cha ufuatiliaji wa familia**'. Ikiwa una mwanafamilia anayeishi katika nchi nyingine ya EU+ na bado hujapokea fomu hii, zungumza na afisa au mshauri wako wa kisheria. Wanaweza pia kukusaidia kujaza fomu hiyo.

Unaweza kupata maelezo ya kina zaidi kuhusu uwezekano wa kuungana tena na wanafamilia katika sehemu yenye kichwa **'Ni ushahidi gani unaweza kutoa kuthibitisha kuwa una familia katika nchi nyingine ya EU+?'**

## 2) Ruhusa ya kuingia nchi maalum ya EU+

Nchi ya EU+ inaweza kuwa na jukumu la kuchunguza ombi Lako ikiwa:



- una viza au kibali cha makazi katika nchi fulani ya EU+
- umeingia nchi ya EU+ ambayo uliruhusiwa kuingia bila viza kwa sababu nchi yako ya nyumbani ina makubaliano na nchi hiyo.

## 3) Sababu ya masomo /diploma



- Umehitimu na kupata cheti au diploma baada ya kusoma ana kwa ana katika taasisi ya elimu katika nchi ya EU+ kwa angalau mwaka mmoja wa masomo.

## 4) Kuingia kinyume cha sheria katika nchi maalum ya EU+

Nchi nyingine ya EU+ inaweza kuwa na jukumu la kuchunguza ombi lako ikiwa:



- Umevuka mpaka wa nje wa mojawapo ya nchi za EU+ bila ruhusa.



- Ulikokolewa baharini na mamlaka ya nchi ya EU+ katika safari yako kuelekea Ulaya



- Umeomba ulinzi wa kimataifa katika eneo la mpito la uwanja wa ndege katika mojawapo ya nchi za EU+.

## 5) Kuwaunganisha tena mlezi na mwanafamilia anayemtegemea

Unategemea utunzaji wa mwanafamilia ambaye yuko katika nchi nyingine ya EU+ au una mwanafamilia katika nchi ya EU+ anayetegemea utunzaji wako.



Mwanafamilia anayetegemea anaweza kuhitaji msaada kwa sababu ya:

- Ujauzito
- Kuzaa  mtoto
- ugonjwa mbaya wa akili au wa kimwili
- ulemavu mkubwa
- mshtuko mkuu wa kisaikolojia
- Uzee.

Katika kesi za utegemezi, ni lazima uweze kuonyesha kuwa unaweza kumtunza mtu anayetegemea au kwamba mwwanafamilia anaweza kukutunza.

## 6) Sababu za kibinadamu

Kunaweza kuwa na sababu ya kibinadamu inayofanya nchi maalum ya EU+ ichunguze ombi lako. Hii inaweza kutegemea misingi ifuatayo:

- mazingatio ya kifamilia
- mazingatio ya kijamii
- mazingatio ya kitamaduni
- Nchi nyingine ya EU+ inaweza kuombwa kuchunguza ombi lako kwa sababu zilizotajwa hapo juu lakini uamuzi wa mwisho utakuwa chini ya mamlaka ya nchi hiyo..

## UNAWEZA KUFANYIWA USAILI ILI KUSAIDIA KUELEWA NI NCHI GANI YA EU+ ITAKAYOCHUNGUZA OMBI LAKO

Ikiwa hii ni mara yako ya kwanza kuomba hifadhi, mamlaka zinapaswa kupanga usaili wa ana kwa ana.

**MAMBO YA KUZINGATIA!** Huu hautakuwa usaili wa hifadhi. Usaili huu unalenga kubaini ni nchi gani ya EU+ inayopaswa kuchunguza ombi lako.

**Usaili huu una ana malengo makuu manne:**

- nchini nyingine ya EU+ au kwa nini uruhusiwe kubaki katika nchkukusanya taarifa zitakazosaidia mamlaka kuamua kuhusu nchi husika ya EU+
- kukuruhusu kuuliza maswali yoyote kuhusu jinsi taratibu za kubaini nchi husika ya EU+ zinavyofanyika
- kukuruhusu kuuliza maswali kuhusu taarifa yoyote katika brosha hii
- kukuuliza kama kuna sababu zozote kwa nini usihamishiwe i hii.

usaili uttafanyika kwa lugha unayoielewa vizuri. Kama huzungumzi Kiingereza, mkalimani atakusaidia kuwasiliana na mamlaka wakati wa mahojiano.



Hakuna taarifa yoyote utakayotoa itakayoshirikiwa na serikali au mamlaka katika nchi yako.

Ikiwa kuna jambo lolote wakati wa usaili ambalo haliko wazi, unaweza kuuliza maswali. Ni muhimu kwako na kwa afisa kuelewa kila kitu, kwa hivyo maswali daima yanakaribishwa.



Sauti ya mahojiano/usaili itarekodiwa na utaonyeshwa muhtasari wa maandishi wa yaliyosemwa.

Ikiwa, baada ya kupokea muhtasari wa maandishi wa mahojiano yako binafsi, na unafikiri kuwa taarifa fulani si sahihi na ungependa kuibadilisha, unaweza kuomba kufanya hivyo.

Ikiwa ni lazima, bado unaweza kutoa nyaraka za ziada baada ya usaili au kutoa sababu gani unaomba kutohamishwa kwenda nchi nyingine ya EU+.

Ikiwa bado una taarifa au nyaraka ambazo bado hujaziwasilisha, lazima uziwasilishe kwa mamlaka.

Unaweza kuziwasilisha kupitia akaunti yako ya kielektroniki kwenye Lango la Ulinzi wa Kimataifa au kwa barua pepe kwa contact@ipo.gov.ie.

## JE, USAILI HUFANYIKA KILA MARAI?

Ikiwa hii ni mara yako ya kwanza kuomba hifadhi, mamlaka bado inaweza kuchagua kutofanya usaili wa ana kwa ana ikiwa:

- nchi ya EU+ inayohusika na kuchunguza ombi lako tayari inajulikana
- wana taarifa za kutosha kuamua ni nchi gani ya EU+ inayohusika na kuchunguza ombi lako
- hapo awali umekosa usaili bila kuwaeleza mamlaka kwa nini haukuweza kuhudhuria
- umefeli kuwasiliana na mamlaka..

Ikiwa usaili haujatayarishwa, unaweza kuiomba. Ikiwa maafisa wanafikiri tayari wana taarifa za kutosha kushughulikia kesi yako, wanaweza kukataa ombi hili lakini ni lazima watoe sababu zao za kutofanya usaili.

## Ni ushahidi gani unaweza kutoa ili kuthibitisha kuwa una familia katika nchi nyingine ya EU+?

Njia bora ya kutoa taarifa kuhusu mwanafamilia wako ni kwa kujaza fomu ya **'kiolezo cha kufuatilia familia'.**

Zaidi ya hayo, toa nyaraka rasmi za serikali zinazoweza kuthibitisha uhusiano wako. Unaweza pia kutoa aina nyingine za ushahidi, kwa mfano ushahidi unaoonyesha kuwa umeendelea kuwasiliana na mwanafamilia wako kama picha, barua pepe au ujumbe mfupi.



Ikiwa huna ushahidi kuhusu uhusiano wenu, mamlaka wanaweza kukuomba mfanye kipimo cha DNA ili kuthibitisha kuwa mna uhusiano.

Unaweza kuunganishwa tena na mwanafamilia wako ikiwa nyote wawili mtatoa tamko kwa maandishi kwamba mnataka kuunganishwa tena. Unapaswa kujaribu kutoa hati hii kwa Kiingereza ikiwa unaweza.

Anza kuandaa taarifa hii mapema iwezekanavyo



Ikiwa una maswali zaidi au unahitaji ushauri kuhusu mchakato wa muungano wa familia, unaweza kuomba msaada kutoka kwa mshauri wa kisheria.

Ikiwa una mwanafamilia katika nchi nyingine ya EU+ lakini umepoteza mawasiliano naye, kuna mashirika yanayoweza kukusaidia kumpata.

Unaweza kuwasiliana na mashirika haya kwa kutumia taarifa zifuatazo:
Shirika la Msalaba Mwekundu la Ireland linatoa usaidizi mbalimbali kwa Waombaji wa Ulinzi wa Kimataifa. Tazama Find Missing Family - Irish Red Cross kwa taarifa kuhusu ufuatiliaji wa familia.

# MCHAKATO UTACHUKUA MUDA GANI?



Mawasiliano kati ya nchi kwa kawaida huchukua kati ya **mwezi mmoja 1** na nusu hadi **miezi mitatu 3**, lakini **inaweza kuchukua muda mrefu** zaidi kulingana na kesi yako.



Ikiwa nchi nyingine ya EU+ itathibitisha kuwa itachunguza maombi yako, utahamishwa ndani ya **miezi 6** tangu tarehe walipokubali ombi la kuhamishwa kwako.




Ikiwa ombi lilikuwa ni kwa sababu una mwanafamilia katika nchi nyingine ya EU+, **uhamisho utapewa kipaumbele.**



Ikiwa kwa **sasa umezuiliwa au utazuiliwa baadaye**, kesi yako **itashughulikiwa kwa haraka**. Uhamisho wako unapaswa kupangwa ndani ya **wiki 5**. Ikiwa uhamisho hautatekelezwa ndani ya **wiki 5**, utaachiliwa kutoka uzuizi. Hata hivyo, uhamisho wako utaandaliwa ndani ya **miezi 6** kuanzia tarehe nchi ya EU+ iliyokubali kuchunguza ombi lako ilipokea ombi hilo.

Ikiwa uko gerezani kwa kutenda uhalifu, muda wa uhamisho unaweza **kuongezwa hadi mwaka mmoja 1.**




**MAMBO YA KUZINGATIA!** Ikiwa utatoroka, kujificha au hushirikiane na mamlaka zinazoratibu uhamisho, **muda wa uhamisho unaweza kuongezwa hadi miaka 3.**

## VITAKUWAJE IKIWA TAYARI UMEOMBA ULINZI WA KIMATAIFA KATIKA NCHI NYINGINE YA EU+? - NINI HUTOKEA BAADA YA UAMUZI KUFANYWA?

Unaruhusiwa kuomba ulinzi wa kimataifa katika nchi moja tu ya EU+. Ikiwa tayari umeomba ulinzi wa kimataifa katika nchi nyingine ya EU+, utarudishwa kwenye nchi ya EU+ inayohusika na kuchunguza ombi lako.

Ikiwa kuna taarifa zinazoonyesha kuwa nchi nyingine ya EU+ ndiyo yenye jukumu la kuchunguza ombi lako, taarifa itatumwa kwa nchi hiyo. Ikiwa nchi hiyo ya EU+ itathibitisha kuwa itachunguza ombi lako, utapewa **uamuzi wa kuhamishwa** unaoonyesha ni nchi gani ya EU+ utakayohamishiwa.

Ikiwa hii si mara yako ya kwanza kuomba ulinzi wa kimataifa, au tayari imeamuliwa kwamba nchi nyingine ya EU+ ndiyo inawajibika kuchunguza ombi lako, mamlaka wanaweza kutokufanyisha usaili wa ana kwa ana.

Hata hivyo, utapata fursa ya kueleza kwa nini hutaki kuhamishwa nchini hiyo au kwa nini unaruhusiwa kubaki katika nchi hii.

Unaweza kupata taarifa kuhusu jinsi ya kutoa taarifa hizi hapa chini akaunti yako ya kielektroniki kwenye Lango la Ulinzi wa Kimataifa au kwa barua pepe kwa contact@ipo.gov.ie.

## NINI HUTOKEA BAADA YA UAMUZI KUFANYWA?

Ukipokea uamuzi wa kuhamishwa kwenda nchi nyingine ya EU+, baadhi ya haki zako zitafutwa, kwa mfano:

- hautapokea **huduma nyingi na aina tofauti za usaidizi**
- hautaruhusiwa **kufanya kazi au kufuata masomo.**

Uhamisho unapaswa kufanyika ndani ya miezi 6 tangu tarehe ambayo nchi ya EU+ ilithibitisha au kukubali kuchunguza ombi lako.Ikiwa umeshtakiwa, kesi yako itashughulikiwa kwa haraka. Uhamisho wako unapaswa kuandaliwa ndani ya wiki 5. Ikiwa uhamisho hautafanyika ndani ya wiki 5, utaachiliwa kutoka uzuizini.

Uhamisho wako bado utapangwa ndani ya miezi 6 kuanzia tarehe ambayo nchi ya EU+ ilithibitisha au kukubali kuchunguza maombi yako.Ikiwa uko gerezani kwa kutenda uhalifu, kikomo cha muda cha uhamisho kinaweza kuongezwa hadi kiwango cha juu cha mwaka 1.

**MAMBO YA KUZINGATIA!** Ikiwa utatoroka au hautashirikiana na mamlaka, **muda wa uhamisho unaweza kuongezwa hadi miaka 3.**

## VITAKUWAJE IKIWA HUKUBALIANI NA UAMUZI WA UHAMISHO?



Ikiamuliwa kuwa nchi nyingine ya EU+ ndiyo yenye jukumu la kuchunguza ombi lako, utapokea **uamuzi wa uhamisho**. Uamuzi huu utakujulisha ni nchi gani utahamishiwa.Ikiwa hukubaliani na uamuzi wa uhamisho, unaweza kutoa sababu zako kwa mahakama.

Hii inaitwa kuwasilisha rufaa. Unapo piga rufaa dhidi ya uamuzi, mahakama au baraza la kisheria litatoa uamuzi wa mwisho.

Kuna sababu tatu tu za kupiga rufaa dhidi ya uamuzi wa uhamisho:

- unadai kuwa kuhamishiwa kwako nchini husika la EU+ kutakuwa kinyume na haki zako za binadamu
- kuna taarifa mpya ambayo haikupatikana wakati wa uamuzi wa uhamisho ambayo ingeweza kuathiri uamuzi huo
- una familia katika nchi nyingine ya EU+ ambayo unapaswa kuunganishwa nayo badala yake.

Ikiwa huwezi kumudu kuajiri mshauri wako mwenyewe wa kisheria, mshauri wa kisheria atapatikana ili kukusaidia na rufaa bila malipo.




Utasaidiwa na mkalimani anayeongea lugha unayoielewa katika mchakato huu wote.

# UNACHOHITAJI KUJUA KUHUSU UTARATIBU WA RUFAA WAKATI ATHARI YA KUSITISHA UTEKELEZAJI NA RUFAA YA MSINGI ZIMETENGANISHWA

Muda wa mwisho, mahali na jinsi ya kuwasilisha rufaa vitaelezwa katika uamuzi wa uhamisho utakaotolewa kwako.

Kwanza, utaombwa kutoa sababu  gani unapaswa kuruhusiwa kubaki katika nchi hii wakati rufaa yako inasubiriwa kuamuliwa. **Hii** inajulikana kama rufaa ya athari ya kusitisha.Mahakama itaamua ndani **ya mwezi mmoja 1** iwapo unaruhusiwa kubaki katika nchi hii wakati rufaa yako inashughulikiwa.

Ikiwa mahakama itaamua kuwa haupaswi kuruhusiwa kubaki katika nchi hii wakati rufaa yako inashughulikiwa, utahamishiwa kwenda nchi ya EU+ inayohusika na kuchunguza ombi lako wakati rufaa yako inashughulikiwa.Ikiwa mahakama itaamua kwamba unaruhusiwa kubaki katika nchi hii wakati rufaa yako inasubiriwa, basi watakuomba utoe sababu gani hukubaliani na uamuzi wa kuhamishwa. Mahakama kisha itajaribu kukupa uamuzi ndani ya **mwezi mmoja 1** tangu uamuzi wa rufaa kuhusu kusitisha utekelezaji

Ikiwa rufaa yako haitakubaliwa, utahamishiwa kwenda nchi ya EU+ inayohusika na kuchunguza ombi lako. Uhamisho huo unapaswa kufanyika ndani wiki 4 tangu tarehe ambayo mahakama ilitoa uamuzi wake wa mwisho.

Ikiwa unazuiliwa kwa sasa au utazuiliwa siku zijazo, kesi yako itashughulikiwa kwa haraka. Uhamisho wako unapaswa kupangwa ndani ya wiki 5. Ikiwa uhamisho hautatekelezwa ndani ya wiki 5, utaachiliwa kutoka kizuizini. Hata hivyo, uhamisho wako bado utapangwa ndani ya miezi 6 kuanzia tarehe nchi ya EU+ inayohusika na kuchunguza ombi lako ilipokubali ombi hilo.

**MAMBO YA KUZINGATIA!** Ni lazima ushirikiane na mamlaka ikiwa nchi nyingine ya EU+ ndiyo inayohusika na kuchunguza ombi ako.

## NI DATA GANI ZA KIBINAFSI ZITAKAZOKUSANYWA?



Maafisa katika nchi ya EU+ unakoishi watakusanya taarifa fulani, ikiwemo zifuatazo:

- Maelezo yako ya kibinafsi na ya wanafamilia wanaosafiri na wewe (jina, uraia, tarehe na mahali pa kuzaliwa). Ikiwa umewahi kutumia majina na maelezo tofauti, watakuuliza kuhusu hilo.
- Taarifa kuhusu utambulisho wako na nyaraka zako za kusafiria.
- Taarifa nyingine yoyote inayoweza kuthibitisha utambulisho wako, kama vile alama zako za vidole.
- Maelezo kuhusu wanafamilia wowote wanaoishi katika nchi nyingine ya EU+, kama vile maelezo yao binafsi, mara ya mwisho mlipowasiliana, eneo lao na hadhi yao ya kisheria.
- Maelezo kuhusu nyaraka zozote ulizonazo ambazo zimekuruhusu kuishi katika nchi ya EU+ ikiwa hali hii inakuhusu..
- Taarifa kuhusu nyaraka zinazoonyesha kuwa ulisoma katika nchi ya EU+ kwa zaidi ya mwaka mmoja.
- Taarifa kuhusu nchi ulizopitia ili kufika katika nchi hii.Hali zako binafsi.
- Tarehe ya maombi yoyote ya awali ya ulinzi wa kimataifa na matokeo ya maombi hayo.

## UNA HAKI GANI KUHUSIANA NA DATA ZAKO ZA KIBINAFSI?

Una haki ya kupata data yoyote uliyowasilisha kwa mamlaka.

Ikiwa unaamini data yako yoyote ya kibinafsi si sahihi au haishughulikiwi kisheria, unaweza kuomba kupata data yako ya kibinafsi kwa kuwasiliana na mdhibiti wa data ili kuomba data isiyo sahihi isahihishwe au data iliyoshughulikiwa kinyume cha sheria ifutwe.

Unaweza kuwasiliana na mdhibiti wa data katika nchi hii kwa kutumia taarifa zilizo hapa chini.
International Protection Office, Immigration Service Delivery, 79-83 Lower Mount Street, Dublin 2, D02 ND99
contact@ipo.gov.ie

Brosha hii itatumiwa kwa madhumuni ya taarifa pekee. Haileti haki wala wajibu wowote. Shirika la Umoja wa Ulaya la Hifadhi (EUAA) limetoa sehemu kuu ya nyenzo hii, na unakili na mabadiliko ya brosha hii yameruhusiwa na EUAA kwa Nchi Wanachama wa Umoja wa Ulaya pekee. EUAA haikubali jukumu lolote au uwajibikaji wowote kwa usahihi, yaliyomo, ukamilifu, kisheria au uaminifu wa taarifa zilizojumuishwa katika brosha hii na Nchi Wanachama wa EU au na mtu mwingine yeyote anayehusika. Wala EUAA wala mtu yeyote anayefanya kazi kwa niaba ya EUAA hawawajibiki kwa matumizi yanayoweza kufanywa ya taarifa zilizomo katika brosha hii.

© Shirika la Umoja wa Ulaya la Hifadhi, 2025